# BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023

## 102 KISWAHILI

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO

DIBAJI........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI........................................................................................1

2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA.......................................................................1

3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI..............................1

3.1. SEHEMU A: UFAHAMU..............................................................................1

3.1.1 : Swali la 1: Ufahamu.............................................................................2

3.1.2 : Swali la 2: Ufupisho wa habari..............................................................4

3.2. SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA.............................................. 6

3.2.1 : Swali la 3: Vipengele vya sarufi ............................................................ 6

3.2.2 :Swali la 4: Vipengele vya sarufi ............................................................. 8

3.2.3 :Swali la 5: Matumizi ya lugha ..............................................................11

3.2.4 : Swali la 6:Kutafsiri na Matumizi ya kamusi...........................................13

3.2.5 : Swali la 7: Matumizi ya lugha na mawasiliano .......................................16

3.3. SEHEMU C: FASIHI..................................................................................18

3.3.1 : Swali la 8: Fasihi andishi......................................................................18

3.3.2 : Swali la 9: Fasihi simulizi .....................................................................22

3.3.3 : Swali la 10: Fasihi andishi ....................................................................24

3.4. SEHEMU D: STADI ZA UTUNGAJI...............................................................28

3.4.1 : Swali la 11: Utungaji wa insha...............................................................28

3.4.2 : Swali la 12: Matangazo ya biashara .......................................................31

4.0 HITIMISHO.............................................................................................34

5.0 MAPENDEKEZO .......................................................................................34

VIAMBATANISHO ......................................................................................... 35

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuingilia Kidato cha Kwanza katika Somo la Kiswahili mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa Kuingilia Kidatu cha Kwanza ni kigezo cha miaka mitatu ya Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi hukusudiwa kupimwa ni kwa namna gani wameweza kukumbuka masomo yao ya Darasa la Tano (5) hadi la Saba (7). Hivyo, mtihani huu ni maandalizi tosha kwa ajili ya Elimu ya Sekondari.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taaarifa hii una lengo la kuelewa kwa undani zaidi sababu ya watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika mtihani wao. Taarifa inathibitisha kuwa baadhi ya sababu zilizopelekea watahiniwa wengi kupata alama za juu katika majibu yao ni pamoja na kuelewa matakwa ya swali husika, uelewa juu ya dhana mbalimbali zilizohusiana na somo la Kiswahili.

Pia, taarifa hii inatuonesha miongoni mwa sababu zilizopelekea baadhi ya watahiniwa kufanya vibaya katika mtihani wao wa somo la Kiswahili mwaka 2023. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na kutoolewa matakwa ya swali husika, muandiko mbaya na usiofahamika pamoja na kushindwa kutoa majibu sahihi.

Aidha, uchamnbuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivojibu vizuri au vibaya. Mwisho, uchambuzi huu umetumia machati ambayo yamebainishwa kwa rangi tofauti. Machati hayo yanaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, Baraza lina imani kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa Elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Kiswahili katika Mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa wa Mitihani na na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**DKt. RASHID .A. MUKKI**



**MKURUGENZI**
**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**
**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa kuingia Kidato cha Kwanza kwa somo la Kiswahili Mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Zanzibar wa mwaka 2009 na 2022 na kufuata muundo wa mtihani wa Darasa la Saba wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2022.

Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali 12 yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C na D. Katika sehemu A kulikuwa na jumla ya maswali mawili na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali matano watahiniwa walitakiwa kujibu maswali manne, Sehemu C ilikuwa na maswali matatu na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali mawili na sehemu D ilikuwa na jumla ya maswali mawili ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu swali moja tu.

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **4,717** sawa na asilimia **10.78** ya watahiniwa **43,755** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri ambapo vibaya ulianza alama 0 hadi 20, wastani 21 hadi 60 na vizuri 61 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia chati/grafu kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B, C na D. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa

### 3.1. SEHEMU A: UFAHAMU

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) yaliyotokana na mada ya ufahamu, ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Swali la kwanza (1) lilikuwa na alama kumi (10) na swali la pili (2) lilikuwa na

alama tano (05). Hivyo katika sehemu hii kulikuwa na jumla ya alama kumi na tano (15).

### 3.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali la kwanza lilitokana na mada ya ufahamu ambapo watahiniwa walitakiwa kuisoma habari waliyopewa na kisha kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo.Swali lilikuwa navipengele vitano (5) kuanzia (a) hadi (e).Swali hili lilikuwa na jumla ya alama kumi (10), kila kipengele kilikuwa na alama mbili (2).

Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kueleza sababu iliyowafanya Sudi na wenzake kuchelewa kurudi baharini (b) kilimtaka mtahiniwa kutaja kazi aliyokuwa wakifanya Sudi na wenzake, kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa aandike kilichotokea katika dau la kina Sudi baada ya kwenda mrama, kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kubainisha mbinu aliyotumia Sudi na wenzake ili kukabiliana na maji yaliyokuwa yakiingia katika chombo chao (e) kilimtaka mtahiniwa kutaja ishara waliyoionesha Sudi na wenzake ili kujulikana kwa urahisi mahali walipo.

Kwa ujumla swali hili lililenga kumpima mtahiniwa katika hali ya *kukumbuka na kuelewa* habari na kujibu maswali kulingana na habari husika.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **4,685** sawa na asilimia **99.32** na watahiniwa **32** sawa na asilimia **0.68** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1a.


**Jadweli nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 560 | 11.95 | 929 | 19.83 | 3,196 | 68.22 | 4,125 | 88.05 |

Takwimu za jaduweli nambari 1a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **68.22** upo katika kiwango kizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **88.05**.

Aidha, watahiniwa **560** sawa na asilimia **11.95** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1

**Kielelezo nambari 1.1 (kibaya)**


**MASWALI**

a) Eleza sababu iliyowafanya Sudi na wenzake kuchelewa kurudi baharini.

Siku moja sudi aliondoka na wasaidizi wake kwenda kuvua wanunuzi wali subiri arudi na samaki ili wapate kitoweo.

b) Sudi na wenzake walikuwa wakifanya kazi gani?

Sudi na wasaidizi wake wamelala chini wakitweta.

c) Dau la kina Sudi lilipatwa na nini baada ya kwenda mrama?

Baada ya muda Sudi na wenzake walipata nafuu walipoulizwa matatizo yaliyowapata Sudi alieleza.

d) Bainisha mbinu aliyoitumia Sudi na wenzake ili kukabiliana na maji yaliyokuwa yakiingia katika chombo chao.


mara walioona mwamba mwengine wakaukwepa hawakukubali kufa kikondoo walipania kupigana kiume ili kuokoa.

e) Taja ishara waliyoionesha Sudi na wenzake ili kujulikana kwa urahisi mahali walipo.

Kielezo nambari 1.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye ameweza kujibu vipengele vyote vya swali la kwanza lakini hakuweza kupata alama kwasababu alikariri baadhi ya sentensi zilizopo kwenye ufahamu aliyopewa badala ya kujibu maswali aliyoulizwa.

Aidha, watahiniwa **3,196** sawa na asilimia **68.22** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa naufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitisha katika kielelezo nambari 1.2.

## Kielelezo nambari 1.2 (Vizuri)



**MASWALI**

a) Eleza sababu iliyowafanya Sudi na wenzake kuchelewa kurudi baharini.

Sababu iliyowafanya sudi na wenzake kuchelewa kurudi baharini kwasababu walikumbwa na dhoruba kali.

b) Sudi na wenzake walikuwa wakifanya kazi gani?

Sudi na wenzake walikua ni wavuvi.

c) Dau la kina Sudi lilipatwa na nini baada ya kwenda mrama?

Tanga lilitaruka na dau likakwama kwenye mwamba.

d) Bainisha mbinu aliyoitumia Sudi na wenzake ili kukabiliana na maji yaliyokuwa yakiingia katika chombo chao.

Sudi na wenzake walipangiana zamu za kutoa maji chomboni.

e) Taja ishara waliyoionesha Sudi na wenzake ili kujulikana kwa urahisi mahali walipo.

Kielelezo nambari 1.2 ni mfano wa mmoja wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa anaonekana kuwa aliisoma habari mwanzo hadi mwisho nakuweza kujibu maswali kwa ufasaha kama yalivyoulizwa.

### 3.1.2 Swali la 2: Ufupisho wa habari

Swali hili lilitokana na mada ya ufahamu na ufupisho na lilimtaka mtahiniwa kuisoma kwa makini habari aliyopewa na kisha kuifupishaaya ya kwanza ya habari hiyo kwa maneno yasiyozidi 20. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 05.

Kwa ujumla swali hili lililenga kumpima mtahiniwa katika hali ya *kuchambua* habari na kujibu maswali kulingana na habari husika.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **4,238** sawa na asilimia **89.85** na watahiniwa **479** sawa na asilimia **10.15** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 1b.


**Jadweli nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 - 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,532 | 59.75 | 1,580 | 37.28 | 126 | 2.97 | 1,706 | 40.25 |

Takwimu za jaduweli nambari 1b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **59.75** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wastani wa asilimia **40.25**.

Aidha, watahiniwa **2,532** sawa na asilimia **59.75** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1

**Kielelezo nambari 2.1 (kibaya)**



2. Fupisha aya ya tatu (3) ya habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

Siku moja sudi aliondoka na ~~marafiki~~ wasaidizi wake kwenda kuvua wanunuzi waliwasubiri ili wapate kitoweo. Siku hiyo haija onekana. Usiku ulipoingia vijana na wazee wakawana wasiwasi walienda pwani na kuwafuta pute ((maneno 20))

Kielelezo nambari 2.1 ni mfano ya jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa huyu badala ya kufupisha aya ya tatu (3) kama swali lilivyomtaka, yeye alirudia sentensi za mwanzo katika aya ya kwanza ya habari aliyopewa.

Aidha, watahiniwa **126** sawa na asilimia **2.97** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitisha katika kielelezo nambari 2.2.

**Kielelezo nambari 2.2 (Vizuri)**


2. Fupisha aya ya tatu (3) ya habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

Sudi na wenzake walikumbwa na dhoruba kali ambayo ilisababisha kuharibika kwa dau lao na kuwagharimu Sudi na wenzake maisha yao.

Kielelezo nambari 2.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyefupisha aya ya tatu (3) ya habari aliyopewa kwa kuzingatia kanuni za ufupisho kama vile kuandika mawazo makuu ya habari, matumizi sahihi ya sentensi, alama na vituo pamoja na kuzingatia idadi ya maneno.

## 3.2. SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali matano (5) yaliyotokana na mada ya sarufi na matumizi ya lugha, ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali manne (4) na hakukuwa na swali la lazima. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na alama (10) na hivyo kufanya jumla ya alama zote kuwa ni arobaini (40).

### 3.2.1 : Swali la 3: Vipengele vya Sarufi

Swali hili lilihusu mada ya sarufi katika kauli za vitenzi (kutendwa) ambalo lilimtaka mtahiniwa kubadilisha sentensi kwenda katika kauli ya kutendwa katika sentensi tano alizopewa. Sentensi hizo ni (a) Paka anakunywa maziwa (b) Fundi alishona viatu vyao (c) Kamaria amekichana kitabu changu (d) Wakulima watavuna mazao mengi mwaka huu na (e) Babu amewasha moto.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *kumbukumbu na ufahamu* alionao mtahiniwa kuhusu kauli za vitenzi katika sentensi.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **4,496** sawa na asilimia **95.31** na watahiniwa **221** sawa na asilimia **4.69** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2a.


**Jadweli nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,609 | 58.03 | 699 | 15.55 | 1,188 | 26.42 | 1,887 | 41.97 |

Takwimu za jaduweli nambari 2a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **58.03** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwa asilimia **41.97**.

Aidha, watahiniwa **2,609** sawa na asilimia **58.03** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1

**Kielelezo nambari 3.1: (kibaya)**


3. Badilisha sentensi zifuatazo kwenda katika kauli ya kutendwa.

a) Paka anakunywa maziwa.

Paka anakunyua maziwa

b) Fundi alishona viatu vyako.

Fundi anashona viatu vyako.

c) Kamaria amekichana kitabu changu.

Kamaria anachana kitabu changu

d) Wakulima watavuna mazao mengi mwaka huu.

Mkulima anavuna mazao mengi mwaka huu.


e) Babu amewasha moto.

Babu anawasha moto.

Kielelezo nambari 3.1ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya na kupata ufaulu wa alama 00. Mtahiniwa huyu amekosa kumbukumbu na ufahamu wa kutosha kuhusu mada ya kauli za vitenzi. Kama inavyojionesha katika kielelezo mtahiniwa amerejea kuziandika sentesi badala ya kubadilisha sentensi kwenda katika kauli ya kutendwa.

Aidha, watahiniwa **1,188** sawa na asilimia **26.42** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitisha katika kielelezo nambari 3.2

**Kielelezo nambari 3.2 (Vizuri)**


3. Badilisha sentensi zifuatazo kwenda katika kauli ya kutendwa.

a) Paka anakunywa maziwa.
Maziwa yananywiwa na Paka.

b) Fundi alishona viatu vyako.
Viatu vyako vilishonwa na fundi.

c) Kamaria amekichana kitabu changu.
Kitabu changu kimechanwa na Kamaria.

d) Wakulima watavuna mazao mengi mwaka huu.
Mwaka huu mazao mengi yatavunwa na wakulima.

e) Babu amewasha moto.
Moto umewashwa na babu.

Kielelezo nambari 3.2ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri vipengele vyote vya swali husika kwa vile mtahiniwa huyu alikuwa na uwelewa wa kutosha juu ya mada ya kauli za vitenzi. Kwa mfano katika kipengele d mtahiniwa ameweza kubadilisha sentensi kwenda katika kauli ya kutendwa. Kipengele ambacho kilikuwa na sentensi yenye maneno mengi kuliko sentesi yeyote katika swali nhusika.

### 3.2.2 Swali la 4: Vipengele vya sarufi

Swali hili lilitokana na mada ya sarufi katika vipengele vya aina za maneno pamoja na uundaji wa sentensi. Swali lilikuwa na vipengele viwili “a” na “b”. Kipengele“a” kilimtaka mtahiniwa aeleze maana ya istilahi alizopewa; istilahi hizo ni (i) Nomino, (ii) Kiunganishi na (iii) Sentensi.

Kipengele “b” cha swali hili kilimtaka mtahiniwa kutunga sentensi ambatano kutokana na sentensi alizopewa; ambazo ni (i) Yeye amejifunza sarufi. Mimi nimejifunza fasihina (ii) Wanafunzi waliofanya vizuri wamepewa zawadi.Wanafunzi waliofeli wamerudia darasa.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *kumbukumbu na ufahamu* alionao mtahiniwa kuhusu kauli za vitenzi katika sentensi.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **4,231** sawa na asilimia **89.70** na watahiniwa **486** sawa na asilimia **10.30** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2b.


**Jadweli nambari 2b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,114 | 26.33 | 1,152 | 27.23 | 1,965 | 46.44 | 3,117 | 73.67 |

Takwimu za jaduweli nambari 2b zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **46.44** upo katika kiwango kizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **73.67**.

Aidha, watahiniwa **1,114** sawa na asilimia **26.33** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1.

**Kielelezo nambari 4.1. (Kibaya)**



4. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo.

i. Nomino

NENO LINALO KUMBUCHA JINA LAMTU AU MNAMA AU KITU

ii. Kiunganishi

BIBI ANASHONGA UGALI WA SEMBE

iii. Sentensi

NIKITU CHI CHENE KUJIFUZA UKAWA MANAKO AUMANAME

b) Unda sentensi ambatano kwa kutumia sentensi zifuatazo.

i. Yeye amejifunza sarufi. Mimi nimejifunza fasihi.

SHOTE TULIJUFUZA MASHOMO YOTE NA TUKAPASIMA SHOMO YOTE

ii. Wanafunzi waliofanya vizuri wamepewa zawadi. Wanafunzi waliofeli wamerudia darasa.

WANAFUZI WALIPASIWOTEKAZI DULA HAKUFAULU MANA HAENDA MASOMOTOTE

Kielelezo nambari 4.1ni mfano ya jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa ameshindwa kujibu kile alichoulizwa. Kwa mfano kipengele cha 4 a (iii) ameandika tungo ambazo hazina maana katika lugha ya Kiswahili akiwa ana maanisha maana ya sentensi.

Vilevile katika kipengele cha 4.b mtahiniwa ameshindwa kutunga sentensi kulingana na maelekezo aliyopewa badala yake amechanganya herufi kubwa na ndogo katika neno moja.

Aidha, watahiniwa **1,965** sawa na asilimia **46.44** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitisha katika kielelezo nambari 4.2.

**Kielelezo nambari 4.2 (Vizuri)**

4. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo.

i. Nomino

Nomino ni maneno yanayoelezea majina ya watu vitu, viumbe au kitu chengine chochote Mfano Juma anatembea.

ii. Kiunganishi

Kiunganichi ni neno au kifungu cha maneno chenye kuunganisha sentensi na Sentensi au aya kwa aya Mfano Baba anasoma na Mama anapika

iii. Sentensi

Sentensi ni neno au kifungu cha maneno chenye kutoa maana kamili, kuna aina 4 za Sentensi mfano wa Sentensi Mama anapika Chakula.

b) Unda sentensi ambatano kwa kutumia sentensi zifuatazo.

i. Yeye amejifunza sarufi. Mimi nimejifunza fasihi.

Yeye amejifunza Sarufi na Mimi nimejifunza fasihi.

ii. Wanafunzi waliofanya vizuri wamepewa zawadi. Wanafunzi waliofeli wamerudia darasa.

Wanafunzi walifanya vizuri wamepewa zawadi na wanafunzi waliofeli wamerudia Darasa.

Kielelezo nambari 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu. Mtahiniwa huyu alifanikiwa vyema kueleza maana ya istilahi alizopewana kuweka mifanovilevile ameweza kutunga sentensi ambatano kutokana na sentensi alizopewa.

### 3.2.3 Swali la 5: Matumizi ya lugha

Swali hili lilitokana na mada ya matumizi ya lugha na kusoma nambari za milango saba.Swali lilikuwa na vipengele viwili “a” na “b”. Kipengele “a” kilimtaka mtahiniwa kueleza dhima za lugha kisiasa na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kuandika nambari kwa kuzingatia alama na vituo kutokana na tarakimu alizopewa, nazo ni; (i) 64967 (ii) 2338512.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *kumbukumbu na ufahamu* alionao mtahiniwa juu ya matumizi ya lugha na kusoma nambari za milango saba.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **3,754** sawa na asilimia **79.58** na watahiniwa **963** sawa na asilimia **20.42** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2c.


**Jadweli nambari 2c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,621 | 43.18 | 1,656 | 44.11 | 477 | 12.71 | 2,133 | 56.82 |

Takwimu za jaduweli nambari 2c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **44.11** upo katika kiwango wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwa asilimia **56.82**.

Aidha, watahiniwa **1,621** sawa na asilimia **43.18** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1

## Kielelezo nambari 5.1: (kibaya)


5. a) Eleza dhima tatu (3) za lugha kisiasa.

i. Kuwa elazima na kidahale katika jumi

ii. Kuwa na Kisaso na Kimagigo

iii. Kusoma na Kufaka Kazifuziri

b) Ziandike nambari zifuatazo kwa kuzingatia alama na vituo.


i. 64967 Elufu Nene, Laki Tisa, na Bitina Saba. Elfu Sata, Laki Tisi Miya

ii. 2338512 Elfu Isiri na Tatu na Samani na Kimi na Tame

Kielelezo nambari 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya kwani mtahiniwa huyu hakuwa na maarifa na ufahamu wa kutosha kuhusu swali aliloulizwa. Kwa mfano katika kipengele (b) mtahiniwa alijarirabu kuandika maneno ya tarkimu alizopewa badala ya kuweka alama na vituo katika nambari.

Aidha, watahiniwa **477** sawa na asilimia **12.71** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitisha katika kielelezo nambari 5.2

**Kielelezo nambari 5.2 (Vizuri)**


5. a) Eleza dhima tatu (3) za lugha kisiasa.

i. Hutumika kudai uhuru : ~~Jat~~ Jamii hutumia lugha katika kudai uhuru wa nchi au wa jambo fulani ili kuleta maendeleo.

ii. Kujenga umoja na mshikamano : kwa kutumia lugha watu wanajenga umoja katika mapinduzi ya vyama vya kisiasa.

iii. Ni nyenzo ya ushindi : Viongozi huwa wanatumia lugha kutangaza sera za vyama na kupata ushindi kutokana na sera zao.

b) Ziandike nambari zifuatazo kwa kuzingatia alama na vituo.

i. 64967

64,967.

ii. 2338512

2,338,512.

Kielelezo nambari 5.1kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri vipengele vyote kwani mtahiniwa huyu aliweza kueleza kwa usahihi dhima za lugha kisiasa kwa ufafanuzi ulio bora katika 5 (a) na pia katika 5 (b) aliweza kuziandika nambari alizopewa kwa kuzingatia alama na vituo.

### 3.2.4 Swali la 6:Kutafsiri na Matumizi ya kamusi

Swali hili lilitokana na mada zakutafsiri matini ya kiingereza namatumizi yakamusi.Swali lilikuwa na vipengele viwili “a” na “b”. Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kutafsiri aya yay a lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya kiingerezana kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kueleza tofauti iliyopo kati ya kidahizo na kitomeo.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *ufahamu na uchambuzi* alionao mtahiniwa juu ya mada za kutafsiri na matumizi ya kamusi.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **3,549** sawa na asilimia **75.24** na watahiniwa **1,168** sawa na asilimia **24.76** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2d.


**Jadweli nambari 2d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 620 | 17.47 | 2,057 | 57.96 | 872 | 24.57 | 2,929 | 82.53 |

Takwimu za jaduweli nambari 2d zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **57.96** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **82.53**.

Aidha, watahiniwa **620** sawa na asilimia **17.47** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1

**Kielelezo nambari 6.1: (kibaya)**



6. a) Tafsiri aya ifuatayo kwa Kiswahili.

I am a student. My father is a doctor and my mother is a teacher. At home I live with my father. I have a white cat at home whose name is Hellen. I love my cat very much. I prepare some milk and some fish for Hellen every morning.

ma student my father is adoctor and
my mo ther is a tra her at home Live
with my father halle awhite
Cat at home name is Hellen
Love my cat Very much par at Some

b) Eleza tofauti iliyopo kati ya kidahizo na kitomeo.


katika wata akwenda kwenda
kwanda gani maadu njoo

makidi mi Ulu ga anizika kiswasi

Haraku ni kafarov matokipa timanwa

Kielelezo nambari 6.1ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali nambari 6. Majibu ya mtahiniwa huyu yanaonesha wazi kuwa hakuwa na ufahamu pamoja na maarifa mazuri kuhusumada za kutafsiri matini ya kiingereza na matumizi ya kamusi kwa mfano katika kipengele cha 6 (a) mtahiniwa amejaribu kuiandika tena aya ya kiengereza badala ya kuitafsiri kwenda lugha ya Kiswahili majibu ambayo hayakuwa sahihi.

**Kielelezo nambari 6.2 (Vizuri)**


6. a) Tafsiri aya ifuatayo kwa Kiswahili.

I am a student. My father is a doctor and my mother is a teacher. At home I live with my father. I have a white cat at home whose name is Hellen. I love my cat very much. I prepare some milk and some fish for Hellen every morning.

Mimi ni mwanafunzi. Baba yangu ni daktari na mama yangu ni mwalimu. Nyumbani naishi na Baba yangu. Nina Paka mweupe nyumbani Jina lake ni Helen. Nampenda Paka wangu sana. Namwandalia maziwa na na samaki kwa Helen kila asubuhi

b) Eleza tofauti iliyopo kati ya kidahizo na kitomeo.

Kidahizo ni maneno yaliyoandikwa katika kamusi kwa chapa iliyokoza. Kitomeo ni maneno au kidahizo pamoja na taarifa zake anazozihitaji mtumiaji wa kamusi

Kielelezo nambari 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali nambari 6 kwani mtahiniwa huyu alikuwa ufahamu pamoja na maarifa mazuri kuhusu mada za kutafsiri matini ya kiingereza na matumizi ya kamusi. Kwa mfano katika kipengele cha 6 (a) mtahiniwa ameweza kutafsiri kwa ufasaha sentensi za aya kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.

**3.2.5 Swali la 7: Matumizi ya lugha na mawasiliano**

Swali hili lilitokana na mada za matumizi ya lugha na mawasiliano.Swali lilikuwa na vipengele viwili “a” na “b”. Kipengele “a” kilimtaka mtahiniwa kueleza michango ya njia za kisasa za mawasiliano katika kuleta maendeleo ya Zanzibar (b) kilimtaka mtahiniwa kutaja faida za lahaja.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *kumbukumbu na ufahamu* alionao mtahiniwa juu ya matumizi ya lugha na mawasiliano.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **2,099** sawa na asilimia **44.50** na watahiniwa **2,618** sawa na asilimia **55.50** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 2e.


**Jadweli nambari 2e: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 2 | | 2.5 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 883 | 42.07 | 626 | 29.82 | 590 | 28.11 | 1,216 | 57.93 |

Takwimu za jaduweli nambari 2e zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **42.07** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwaasilimia **57.93**.

Aidha, watahiniwa **883** sawa na asilimia **42.07** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wakutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1

**Kielelezo nambari 7.1 (Vibaya)**


7. a) Eleza michango mitatu (3) ya njia za kisasa za mawasiliano katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.

i. michango ya Kisiasa

ii. michango ya Kislamu

iii. michango ya Kiutamaduni

b) Taja faida mbili (2) za lahaja za Zanzibar.


i. Lahaja nyepesi

ii. Lahaja nzito

Kielelezo nambari 7.1ni mfano ya jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa ameshindwa kujibu kile alichoulizwa.Kwa mfano kipengele cha 7 (a) ameandika aina ya michango iliyopelekea maendeleo ya lugha badala ya michango ya njia kisasa za mawasiliano katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.Vilevile katika kipengele cha 7 (b) mtahiniwa ametaja aina za najisi.

Aidha, watahiniwa **590** sawa na asilimia **28.11** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitisha katika kielelezo nambari 7.2

**Kielelezo nambari 7.2 (Vizuri)**


7. a) Eleza michango mitatu (3) ya njia za kisasa za mawasiliano katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.

i. Kuwaunganisha watu wa mataifa mbalimbali.

ii. Hurahisisha masuala ya elimu.

iii. Kutumia muda mfupi katika kuwasili sha taarifa.

b) Taja faida mbili (2) za lahaja za Zanzibar.

i. Hupamba lugha.

ii. Huongeza msamiati katika lugha.

Kielelezo nambari 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama za juu. Mtahiniwa huyu alifanikiwakueleza michango ya njia za kisasa za mawasiliano katika kuleta maendeleo ya Zanzibarna faida za lahaja za Zanzibar.

### 3.3. SEHEMU C: FASIHI

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) yaliyotokana na mada ya fasihi simulizi na fasihi andishi ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali mawili (2) tu na kila swali lilikuwa na alama 15 hivyo jumla ya alama zote katika sehemu hiikuwa ni 30.

#### 3.3.1 Swali la 8: Fasihi Andishi

Swali hili lilitokana na mada ya fasihi andishi (mashairi).Swali lilikuwa na vipengele viwili "a" na "b". Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana

ya mashairi, (b) kilimtaka mtahiniwa kutunga shairi linalozungumzia athari za kuporomoka kwa maadili Zanzibar.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *ufahamu na uundaji* alionao mtahiniwa juu ya mada ya mashairi.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **2,750** sawa na asilimia **58.30** na watahiniwa **1,967** sawa na asilimia **41.70** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3a.

**Jadweli nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,323 | 48.11 | 936 | 34.04 | 491 | 17.85 | 1,427 | 51.89 |

Takwimu za jaduweli nambari 3a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **48.11** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwa asilimia **51.89**.

Aidha, watahiniwa **1,323** sawa na asilimia **48.11** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1

**Kielelezo nambari 8.1 (Vibaya)**

8. a) Nini maana ya mashairi?

Harakaharaka walituretatanga Lahakiba na kuelekea kurenye kisiwa cha karibu maji yaliajaakuingia kurenye chombo chao kumbe chombo kilikuwa kime pata ufa mara waliona mwamba mkubwa wakati ufwepa Hawa kukubali kufa kikondo wakapania kupigana

b) Tunga beti nne (4) za shairi linalozungumzia athari za kuporomoka kwa maadili ya kizanzibari.

1) Naliandika Shairi kuiyeleza dunia jambo hili la Hatari watu wanajifanya vidume wala jabari maa swa wajifanya kwapamoja tusimame jangahili kuondoa

2) leo kuna majaban wana mwanachi jalia tutlikosa sasha un ndani yagote jamii leo natoboa siri ukwali nina usema kweli hadi asikani wageni karakina mana kwapamoja tusimame jangahili kuondoa.

3) Tukifika mashairini wana funzi tuwasachi tuwa fundishe uneni waku semadontachi wasijeshi kwa mwilini Hasa sehemu za siri kwapamoja Tusimame jangahili kuondoa

4) Ukeipata Habari unawezajitilia watu wame panda ani ushoga kujitenda walivulana Hatari wote wa meshari ingiya kalikataza kahari ni mola wetujali kwapamoja tusimame jangahili kuondoa.

Kielelezo nambari 8.1ni mfano ya jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa ameshindwa kujibu kile alichoulizwa.Kwa mfano kipengele cha 8 (a) ameandika baadhi ya sentensi zilizopo katika habari ya swali la kwanza (1) badala ya kuandika maana ya mashairi.

Aidha, watahiniwa **491** sawa na asilimia **17.85** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitika katika kielelezo nambari 8.2

**Kielelezo nambari 8.2 (Vizuri)**

8. a) Nini maana ya mashairi?

Mashairi ni utanzu wa fasihi wenye mpangilio maalumu wa vina na mizani, mishororo, kibwagizo pamoja na kutumia lugha ya mkato inayoelezea wazo/jambo kuhusu mwanaadamu na mazingira yake.

b) Tunga beti nne (4) za shairi linalozungumzia athari za kuporomoka kwa maadili ya kizanzibari.

1. Bismillahi nasoma, kwa jina lake manani
Anayetufunza mema, na kuumba kila shari
Katuhimiza kusoma, si kuranda mitaani
Ukosefu wa nidhamu, waharibu maadili

2. Nguvukazi twaikosa, kwa tamaa mbaya sana
Zanzibari ya sasa, yadumaa kwa vijana
Na wale wengi kabisa, tegemeo la maana
Ukosefu wa nidhamu, waharibu maadili.

3. Vijana wavuta bangi, na sigara vijiweni
Twapata wagonjwa wengi, na vifo vingi nchini:
Twaacha yaliyo mengi, twaingia hatarini.
Ukosefu wa nidhamu, waharibu maadili

4 Nawasii kwa upendo, mutafakari jamani
Mdogo mdogo mwendo, twadidimia nchini.
Tuyafanye kwa vitendo, ya kheri kwetu jamani
Elimu ndio mwenendo, funguo ya maishani
Ukosefu wa Nidhamu, waharibu maadili.

Kielelezo nambari 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali nambari 8 na kupata ufaulu mzuri. Mtahiniwa huyu alikuwa na ubunifu uliomuwezesha kutunga shairi la beti nne (4). Kwa mfano katika kipengele (b) mtahiniwa ametunga lililozungumzia athari za kuporomoka kwa maadili

ya Zanzibar. Shairi ambalo lenye muundo wa kimapokeo lililojengeka kwa vina, mizani, ubeti na kituo.

### 3.3.2 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali hili lilitokanana mada ya fasihi simulizi katika kipengele cha Methali.Swali lilikuwa limtaka mtahiniwa kutoa maana ya maana ya methali zifuatazo (i) Mcheza kwao hutunzwa (ii) Usiache mbachao kwa msala upitao (iii) Pilipili usiyoila inakuwashia nini? (iv) Hamadi kibindoni silaha mkononi (v) Fadhila za punda ni mateke.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *ufahamu* alionao mtahiniwa juu ya mada ya methali.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **2,898** sawa na asilimia **61.44** na **1,819** sawa na asilimia **38.56** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3b.


**Jadweli nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,656 | 57.14 | 972 | 33.54 | 270 | 9.32 | 1,242 | 42.86 |

Takwimu za jaduweli nambari 3a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **57.14** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwaasilimia **42.86**.

Aidha, watahiniwa **1,656** sawa na asilimia **57.14** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1

**Kielelezo nambari 9.1 (Vibaya)**


9. Lete maana ya methali zifuatazo.

i. Mcheza kwao hutunzwa.

ASEO Cheza Kwao hatungwi

ii. Usiache mbachao kwa msala upitao.

usiache ukionacho msala upitao

iii. Pilipili usiyoila inakuwashia nini?

Pili pili unayoila Hakuashia

iv. Hamadi kibindoni silaha mkononi.

MOHD KIBIndani silaha mguni

v. Fadhila za punda ni mateke.

Shugrani ya Punda mateke

Kielelezo nambari 9.1 ni mfano wa jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa ameshindwa kujibu kile alichoulizwa. Kwa mfano kipengele cha (i) na (iv) mtahiniwa ameandika kinyume badala ya maana ya methalializopewa.

Aidha, watahiniwa **270** sawa na asilimia **9.32** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitika katika kielelezo nambari 9.2

**Kielelezo nambari 9.2 (Vizuri)**

9. Lete maana ya methali zifuatazo.

i. Mcheza kwao hutunzwa.

Methali hii inamaanisha kwamba mtu ambaye yuko karibu na ndugu zake au watu wa kwao hupewa upendo na hutunzwa.

ii. Usiache mbachao kwa msala upitao.

Methali hii inamaanisha kwamba mtu unatakiwa usije ukajiharibia jambo kwa kitu cha kupita tuu (Yaani mpano tatizo au shida ya kupita tuu)

iii. Pilipili usiyoila inakuwashia nini?

Hii ina maana kwamba jambo ambalo analipanga mwenzako wewe linakukerea nini. ~~Uta~~(Unatakiwa usifuatilie yasiyokuhusu.)

iv. Hamadi kibindoni silaha mkononi.

Hii ina maana kwamba mtu akijikwa na tatizo huwa na kikingio mkononi.

v. Fadhila za punda ni mateke.

Methali hii maana yake ni fadhila za mtu uliompanyia wema na alopo akakudharau.

Kielelezo nambari 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali nambari 9. Mtahiniwa huyu alikuwa na ufahamu wa mada na matakwa ya swali. Kwa mfano kipengele (ii) na (iii) ameweza kutoa mfano wa maana ya methali husika.

### 3.3.3 Swali la 10: Fasihi Andishi

Swali hili lilitokana na mada ya fasihi andishi katika kipengele cha hadithi fupi na lilikuwa na vipengele vitatu (3); (a) (b) na (c). Mtahiniwa alitakiwa katika kipengele (a) kueleza kwa ufupi dhana ya hadithi fupi, (b) kuandika sifa za hadithi fupi na (c) kueleza dhima za hadithi fupi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima *ufahamu na uchambuzi* alionao mtahiniwa juu ya hadithi fupi.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **3,006** sawa na asilimia **63.73** na **1,711** sawa na asilimia **36.27** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 3c.


**Jadweli nambari 3c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,157 | 38.49 | 1,039 | 34.56 | 810 | 26.95 | 1,849 | 61.51 |

Takwimu za jaduweli nambari 3c zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **38.49** upo katika kiwango kibaya na wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwaasilimia **61.51**.

Aidha, watahiniwa **1,157** sawa na asilimia **38.49** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1.

## Kielelezo nambari  10.1: (kibaya)


10. a) Eleza kwa ufupi dhana ya hadithi fupi.

kulikua na sadi wakitwe nda kuwa samaki bahati mbaya ikamesha mwa a kubwa na upepo kali uka nzo kuvuma dau lao lika za kwanda maji

b) Andika sifa tano (5) za hadithi fupi.

i. kua kuajasiria kwe za lajiako
ii. wenye wo. kuepo kwa ujasiri wa kupo
iii. kujifua kama wakti kwene kisiwa
iv. kui pepea mashati kwa kati kati umbo
v. lot kuepo kwa kutumia ujanja wao

c) Eleza dhima tano (5) za hadithi fupi.

i. kuepo na kujua kujokoa kutumia ujasiri wa hali
ii. kutumia ujanja wakupepea mashati ta kutumia akili zakuonga kugawa mashati ta fuatayo
iii. kutumia ujanja wa kujitoka kwenye matumbwa
iv. kwanyanyua mashati kuyu lika kwa wako hapa na kuja saidia
v. na mtu mbwa watwa kazi na kwe coto kwe nyekesicha mchango kidoga

Kielelezo nambari 10.1 ni mfano wa jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa alishindwa kujibu kile alichoulizwa. Kwa mfano katita vipengele vyote vitatu (3) mtahiniwa aliandika sentensi zilizopo  kwenye ufahamuwa swali la kwanza (1).

Aidha, watahiniwa **810** sawa na asilimia **26.95** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa  kama inavothibitika  katika kielelezo  nambari 10.2

**Kielelezo nambari 10.2 (Vizuri)**

10. a) Eleza kwa ufupi dhana ya hadithi fupi.

Hadithi fupi ni utanzu wa fasihi unaowasilishwa kwa maandishi na unaomuelezea mwanadam na mazingira yake na huwa na kisa kikuu kimoja

b) Andika sifa tano (5) za hadithi fupi.

i. Huwa na kisa kikuu kimoja
ii. Huwa na wahusika
iii. Huwa na mandhari
iv. Huwa na mwanzo, kati na mwisho
v. Huwa na Huandikwa au kusimuliwa

c) Eleza dhima tano (5) za hadithi fupi.

i. Kuelimsha: hadithi huwa na ujumbe ambao huelimisha jamii au watu kuhusu jambo fulani
ii. Kukosoa: Baadhi ya hadithi huwa na dhima ya kukosoa jambo fulani mfano hadithi zinazohusu uzalilishaji
iii. Kuburudisha: Huwa ina kisa kisa ambacho huburudisha wasomaji wa hadithi
iv. Kufunza: Hadithi fupi nyingi huwa zina mafunzo ndani yake kwa mfano hadithi ya sungura inatufunza tuache wizi
v. Kuonya: Hadithi fupi huwa na lengo la kuonya kwa mfano hadithi za uzalilishaji zinaonya kuacha vitendo hivyo

Kielelezo nambari 10.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali nambari 10. Mtahiniwa huyu alikuwa na ufahamu wa mada na matakwa ya swali. Kwa mfano katika kipengele (c) aliweza kueleza dhima za hadithi fupi na kutoa mifano.

### 3.4. SEHEMU D: STADI ZA UTUNGAJI

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali mawili (2) yaliyotokana na mada ya utungaji ambapo watahiniwa walitakiwa kujibu swali moja (1) na kila

swali lilikuwa na alama 15 hivyo jumla ya alama zote katika sehemu hii ni 15.

### 3.4.1 Swali la 11: Utungaji wa Insha

Swali hili lilitokana namada ya stadi za utungaji hasa katika kipengele cha uandishi waInsha. Swali hili lilikuwa nila kujitegemea na lilimtaka mtahiniwa aandike Insha ya maneno kati ya 120 - 150 kuhusu ajali za barabarani.

Swali hili lililenga kupima hali ya *uundaji* alionao mtahiniwa juu ya uandishi wa Insha.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **1,697** sawa na asilimia **35.98** na **3,020** sawa na asilimia **64.02** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4a.


**Jadweli nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 761 | 44.84 | 533 | 31.41 | 403 | 23.75 | 936 | 55.16 |

Takwimu za jaduweli nambari 4a zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **44.84** upo katika kiwango kibaya ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni wa wastani kwaasilimia **55.16**.

Aidha, watahiniwa **761** sawa na asilimia **44.84** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.1

**Kielelezo nambari 11.1: (kibaya)**



11. Andika Insha isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 150 yenye kichwa cha habari "Ajali za Barabarani".

paukwe! pakawa Hapo zamani za kale palikuwepo Kobe na nyani. Kobe alimualika nyani kuwandaa karamu nyani aliuliza karamu itafanyika wapi. Kobe ~~Alimjibu kwa~~ Hakumjibu. Siku ilipofika Nyani alienda mpaka kwa Kobe, ~~kob~~ Nyani alimuona kobe juu ya mti, nyani akauliza rafiki yangu Kobe karamu itafanyika wapi? Kobe alimjibu karamu juu ya mti, Huko juu ya mti kulikuwa na vinywaji vizuri na vyakula vya aina mbali mbali, Kobe alimwambia nyani apande juu mti nyani alipanda juu ya mti lakini hakuweza kupanda ~~Alibaki huko huko~~ Nyani alianguka na kubaki kulia. Kobe alicheka na kula vyakula vyakula vyote. tangu siku hiyo Nyani na kobe urafiki uliishia Hapo.

Kielelezo nambari 11.1ni mfano wa jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa alishindwa kujibu kile alichoulizwa. Mtahiniwa aliandika hadithi ya kubuni badala ya insha inayohusu ajali za barabarani.

Aidha, watahiniwa **403** sawa na asilimia **23.75** walipata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitika katika kielelezo nambari 11.2

## Kielelezo nambari 11.2 (Vizuri)

11. Andika Insha isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 150 yenye kichwa cha habari "Ajali za Barabarani".

AJALI ZA BARABARANI

Ajali za barabarani ni ajali ambazo hutokea pale watu wasipojua sheria na kanuni za barabarani. Pia ajali hizi husababishwa na madereva wasiokuwa makini na kutokufuata sheria za barabarani. Sababu zinazopelekea ajali za Barabarani ni kama zifuatazo.

Madereva kutokuwa makini: hii inapeleke ajili za barabara kwa uzembi mfano dereva ndani ya gari anazungumza na simu au amelewa sana anasababisha kutokuwa makini katika uendeshaji wake.

Madereva kutokujua alama za barabarani: pia ajili za barabarani humgezeka kwa madereva kutokujua alama za barabarani kwa mfano ameona mbele kuna sehemu ya kuvuka watu yeye anaengeza kasi ya gari na kutokea ajili.

Madereva kuendesha gari kwa mwendo wa kasi: hii pia masababisha ajali za barabarani kwani huwezi ukajua kuwa mbele kuna kitu gani nawewe huku umelewa na gari umetiwa mwende wa kasi unaweza kusababisha ajali za barabarani.

Pia kuna hasara ambazo tunazipata katika ajali za barabarani nazo ni.

~~Watu~~ Watu kupoteza maisha: pale ambapo huko makini unaweza kusababisha ajili ~~nyi~~ nyingi barabarani.

Fedha za Serikali hutumika sana kwa kuwatibia wangonjwa wa ajali za barabarani: hii ni pale ambapo ajali zimekuwa nyingi sana serikali itabidi kufanya juu chini ili wale watu wapate huduma, fedha ile ilikuwa Ikafanyiwe shughuli nyengine lakini inatumika katika huduma

Pia kuna njia za kufuata ambazo zitapungua ajali za barabarani nazo ni.

Kujua vitu na alama za barabarani: ukijua na kufuata alama za barabari ~~ta~~ ajali za barabari zitapungua sana.

Kupunguza mwende wa kasi barabarani: ukiendesha gari yako kwa utaratibu barabara ajali za barabarani zitapungua.

Kuwa na umakini wakiti wa kuendesha gari: ukiendesha gari usiwe umelewa wala usiongee na simu na ~~u~~ usiendeshe mwende wa kasi ili uwe makini katika uendeshaji wako pia ajali za barabarani zitapungua.

Kwa hiyo ninaiyomba serikali kushughulikia juu ya ajili za barabari na pia kuwapa adhabu kali ambao watasababisha ajali za barabarani kwa uzembe.

Kielelezo nambari 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwani mtahiniwa huyu aliweza kutunga Inshailiyokwenda sambamba na mada husika, idadi ya maneno pamoja na kuzingatia taratibuza uandishi wa Insha kama vile kuwa na kichwa cha Insha, utangulizi wa Insha, kiini na hitimisho.

### 3.4.2 Swali la 12: Matangazo ya biashara

Swali hili lilitokana na mada ya stadi za utungaji hasa katika kipengele cha matangazo ya biashara. Mtahiniwa alitakiwa kuandaa tangazo la biashara ya nguo za kitoto kwa njia ya gazeti.

Swali hili lililenga kupima hali ya *uundaji* alionao mtahiniwa juu ya uandishi wa tangazo la biashara.

Swali hili lilijibiwa na wathiniwa **2,406** sawa na asilimia **51.01** na **2311** sawa na asilimia **48.99** hawakujibu swali husika. Uchambuzi wa ufaulu wa wathiniwa unaonekana katika jadweli nambari 4b.


**Jadweli nambari 4b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 – 3 | | 3.5 - 9 | | 9.5 - 15 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 432 | 17.96 | 1101 | 45.76 | 873 | 36.28 | 1974 | 82.04 |

Takwimu za jaduweli nambari 2d zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **45.76** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa ni mzuri wa asilimia **82.04**.

Aidha, watahiniwa **432** sawa na asilimia **17.96** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hao wanaonekana hawakuwa na ufaulu wakutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.1

**Kielelezo nambari 12.1: (kibaya)**



Tangazo Tunauza mabaibu na madira yatoka
omani pambe tu na bainapu kabisa kama vile.
mabaibu Efu kuminatano, madira Efu Sita tu na
tunapatikana hapo michina manzo Namba ya Simu
07614124.

Asateni


baheri

Karibuni

Kielelezo nambari 12.1ni mfano wa jibu la mtahinwa aliyejibu vibaya na kupelekea alama za chini. Mtahiniwa alijitahidi kuandika tangazo la biashara lakini hakuweza kujibu kile alichoulizwa, aliandika bidhaa za watu wazima kama vile madira na mabaibui badala ya bidhaa za kitoto kama alivyotakiwa kwenye swali.

Aidha, watahiniwa **873** sawa na asilimia **36.28** walipata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao wanaonekana walikuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavothibitika katika kielelezo nambari 12.2

**Kielelezo nambari 12.1: (kizuri)**



12. Andaa tangazo la biashara ya nguo za kitoto kwa njia ya gazeti.

TANGAZO

KIBOSHO SHOPPING

Ni wauzaji wa nguo za kitoto za kike na kiume jumla na reja reja. Wanapatikana Mwoa mkabala na skuli ya Mtoni. Wanafungua kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni.

Wasiliana nao kupitia namba zifuatazo

0771037798

AU

9008769789

NYOTE MUNAKARIBISHWA WABILLAHI TAWFIQ

Kielelezo nambari 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu aliweza kuandika barua kama maelekezo ya swali hili yalivyomtaka kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa matangazo ya biashara kama vile kichwa cha habari, kutaja aina ya biashara, aina za bidhaa, bei, mahali inapopatikana huduma na kutaja namna ya kuwasiliana. Hivyo kufanikiwa kupata alama za juu katika swali hili.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali matano (5) yalijibiwa vizuri, maswali saba (7) yalijibiwa wastani na hakuna swali lililojibiwa vibaya.

Mwisho taarifa hii ya watahiniwa kuhusu ufaulu wa watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili na kutoa mrejesho kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali na kuzielewa vizuri ili kufanya marekebisho kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili darasa la Saba inapendekezwa kuwa;

(a) Wanafunzi wahamasishwe kujishughulisha zaidi katika stadi za utunzi wa kazi za fasihi andishi.

(b) Walimu watoe mazoezi / majaribio mengi yanayohusu mada mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa ufahamu wanafunzi utakaowawezesha kwenda sambamba na matakwa ya maswali mbalimbali.

(c) Walimu wawe karibu zaidi na wanafunzi kwa kuwapa kazi mbalimbali ambazo zitainua uwezo wao wa kuandika sentensi zenye kusomeka kwa urahisi.

(d) Walimu wahakikishe kuwa wanamaliza muhutasari wa somo mapema iwezekanavyo ili kupata muda mzuri wa kuwaandaa wanafunzi kwa mtihani.

## VIAMBATANISHO

### KIAMBATANISHO NAMBARI 1

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2023

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | UFAHAMU | 1 | 88.05 | VIZURI |
| 2 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 6 | 82.53 | VIZURI |
| 3 | STADI ZA UTUNGAJI | 12 | 82.04 | VIZURI |
| 4 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 4 | 73.67 | VIZURI |
| 5 | FASIHI | 10 | 61.51 | WASTANI |
| 6 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 7 | 57.93 | WASTANI |
| 7 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 5 | 56.26 | WASTANI |
| 8 | STADI ZA UTUNGAJI | 11 | 55.16 | WASTANI |
| 9 | FASIHI | 8 | 51.89 | WASTANI |
| 10 | FASIHI | 9 | 42.86 | WASTANI |
| 11 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 3 | 41.97 | WASTANI |
| 12 | UFAHAMU | 2 | 40.25 | WASTANI |

### KIAMBATANISHO NAMBARI 2

### UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2022

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 6 | 89.81 | **VIZURI** |
| 2 | UFAHAMU | 1 | 84.66 | **VIZURI** |
| 3 | STADI ZA UTUNGAJI | 12 | 63.00 | **VIZURI** |
| 4 | FASIHI | 10 | 47.94 | **WASTANI** |
| 5 | FASIHI | 8 | 41.69 | **WASTANI** |
| 6 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 4 | 41.33 | **WASTANI** |
| 7 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 3 | 36.89 | **WASTANI** |
| 8 | UFAHAMU | 2 | 32.86 | **WASTANI** |
| 9 | STADI ZA UTUNGAJI | 11 | 32.48 | **WASTANI** |
| 10 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 7 | 28.49 | **WASTANI** |
| 11 | SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA | 5 | 27.76 | **WASTANI** |
| 12 | FASIHI | 9 | 19.80 | **VIBAYA** |